# JARIDA LA

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

*Wizara ya Furaha*

**Toleo la Mtandaoni: 03** | 05 Agosti, 2022 - TABORA | www.michezo.go.tz

# MASHINDANO YA UMITASHUMTA 2022 YAENDELEA KURINDIMA TABORA



Wizara_SanaaTz

# MASHINDANO YA MICHEZO YA UMITASHUMTA YAENDELEA KURINDIMA TABORA

05 Agosti, 2022



# Sanaa za Maonesho Zaendelea Kurindima UMITASHUMTA Tabora

Na Shamim Nyaki - **WUSM**

Katika mashindano ya michezo ya Shule za Msingi ( UMITASHUMTA) yanayoendelea Tabora, Sanaa za jukwani ni sehemu ya mashindano hayo.

Asubuhi ya Agosti 05, 2022 katika ukumbi wa Chuo Cha Ualimu Tabora, mashindano ya Ngoma za mikoa mbalimbali katika hatua ya Makundi yalirindima kwa vijana kuonesha utamaduni wa makabila ya Tanzania.

Wanafunzi kutoka Mikoa ya Tanga, Pwani, Tabora, Rukwa, Simiyu wameonesha vipaji vya hali ya juu kupitia nyimbo za kuhamasisha Sensa ya watu na makazi mwaka huu, pamoja na nyimbo zinazoimbwa katika matukio mbalimbali ya mikoa hiyo.

# YALIYOJIRI LEO KATIKA MASHONDANO YA SANAA ZA NGOMA KATIKA MASHINDANO YA UMITASHUMTA 2022 KATIKA UKUMBI WA CHUO CHA UALIMU TABORA










Ofisi ya
kwa kushirikiana na
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
pamoja na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo
UMITASHUMTA & UMISSETA 2022


UMITASHUMTA & UMISSETA 2022


kwa kushirikiana na
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
pamoja na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo
UMITASHUMTA & UMISSETA 2022


UMITASHUMTA & UMISSETA 2022



# Mwanza na Katavi watangulia Nusu Fainali Wavu

Na Shamim Nyaki - **WUSM**

Timu ya Mkoa wa Mwanza na Katavi ya mpira wa Wavu kwa wavulana wametangulia hatua ya nusu fainali kwa kuibuka washindi kwa seti 3 kwa 2 dhidi ya wapinzani wao katika Mashindano ya UMITASHUMTA mwaka 2022 Mkoani Tabora.

Katika mchezo uliokua na msisimko na upinzani wa hali ya juu uliochezwa Agosti 05, 2022 katika viwanja vya Tabora Sekondari, Mkoa wa Mwanza umeigaragaza Mkoa wa Mara Jumla ya Seti 3 dhidi ya 2.

Watazamaji wa machine hiyo kali wameshuhudia vipaji na uwezo wa hali kutoka kwa timu hizo mbili.

Mchezo mwingine ni kati ya Katavi dhidi ya Mtwara, ambapo Katavi wamewaburuza Mtwara kwa Seti 3 dhidi ya 2.

Kwa matokeo hayo Mwanza na Katavi wametangulia hatua ya Nusu fainali.



# Nusu Fainali ya kwanza Wavu Wasichana kuwakutanisha Dar es Salaam na Mbeya

Na Shamim Nyaki - **WUSM**

Mchezo wa mpira wa Wavu kwa Wasichana katika Mashindano ya UMITASHUMTA mwaka 2022 yamefikia hatua ya Nusu Fainali.

Katika mchezo uliochezwa mapema Agosti 05, 2022 uwanja wa Sekondari ya Tabora Wavulana Mkoa wa Mbeya umeigaragaza Lindi kwa Seti 3 kwa 0.

Mchezo mwingine ni kati ya Dar es Salaam na Manyara ambapo watoto wa mjini Bandari Salama wameonesha uwezo wao kwa watoto wa ukanda wa madini ya Tanzanite na vipaji vya Riadha kama Aliphonce Simbu baada ya kupata Seti 3 dhidi ya 2.

Kwa matokeo hayo timu hizo zitasubiri mshindi atakepatikana katika mechi za jioni kwa ajili ya hatua ya Nusu fainali.



# Mashindano ya Riadha Mbio za Mita 100 na 400 Yashika Kasi

Na Shamim Nyaki - **WUSM**

Mashindano ya Riadha yashika kasi katika Mashindano ya Michezo kwa Shule za Msingi Tanzania.

Agosti 04, 2022 Mchezo wa Riadha kwa Mbio za Mita 100 na 400 zimefanyika kwa wavulana na wasichana na kufikia hatua ya Nusu fainali.

Mbio hizo zitaendelea Agosti 05 katika hatua ya fainali.








422
410
085


422
387
0853

# FAINALI YA KWAYA KATIKA MASHINDANO YA MICHEZO KWA SHULE ZA MSINGI TANZANIA (UMITASHUMTA) YAMEFANYIKA AGOSTI 05, 2022 KATIKA UKUMBI WA TTC TABORA.






Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
pamoja na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo
UMITASHUMTA & UMISSETA 2022


UMITASHUMTA & UMISSETA 2022

# UMITASHUMTA | UMISSETA
# 2022

# #SensaBika

Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo

www.michezo.go.tz